Songcontest

www.uhuru-freiheit.com

Uhuru ni kua huru!

Uhuru means Freedom!

Shiriki kwenye shindano hili!
Kutokana na adhimisho la miaka 60 ya Uhuru wa Tansania, Mission eine EineWelt imeamua kufanya hili shindano ili kupata Wimbo wa Uhuru kutoka Ujerumani na Tansania. Shindano hili linaanza September 2021. Mwisho wa kutuma wimbo wako kuhusu Uhuru ni Tarehe 31.12.2021! Wanaoweza kushiriki ni watu kuanzia miaka 15 na zaidi kutoka Tanzania na Ujerumani!
Tunga wimbo kuhusu Uhuru au Uhuru ni kua huru na kututumia. Nyimbo bora kuliko zote zitawekwa kwenye mitandao yetu na hivyo kuwafikiwa watu wengi duniani kote. – hii ni nafasi yako nzuri ya kutoka haswa kama msanii chipukiz au msanii binafsi.

Vigezo

Washiriki:	Watu Binafsi au Kikundi ama Bendi
Umri:	kuanzia miaka 15 na zaidi.
Muda:	Mwisho wa kutuma wimbo ni tarehe 31. Disemba 2021

Washiriki
Watume wimbo wao waliotunga na kuimba kwa njia ya video kama mp4. Wimbo unaweza kurekodiwa hata kwa kutumia Simu ya mkononi ikiwa imelazwa, kisha pakia kwenye hii tovuti https://uhuru-freiheit.com

Mada yenyewe!

Uhuru ni mada ambayo inatuhusu kila siku. Je, uhuru unamaanisha nini kwangu? Je, kila mtu yuko huru sawa? Ninautumiaje uhuru wangu? Tuna uhuru kiasi gani? Ni wakati gani Uhuru wetu unazuiliwa? Vijana wanawaza nini wakifikiria uhuru wao siku za usoni. Nini maono yao na mipango?

Ni miaka 60 ya uhuru nchini Tanzania - miaka 60 huru kutoka ukoloni. Uhuru huu unauonaje? Zamani ulichukuliwaje? Vijana wa Kitanzania wanauchukuliaje leo?

Mission EineWelt
Weil es uns bewegt!

Watu wa Tanzania na Ujerumani wanachukulia vipi Uhuru huu kwa mwaka huu muhimu wa adhimisho?

Tukiangalia mada ya Uhuru kwa umakini zaidi, tunatambua ya kua: Uhuru wa mtu ni kitu cha thamani sana! Kua huru na kuishi huru sio kitu cha kuchukulia poa.

Zoezi: Ujumbe wa wimbo

Andika wimbo wako kuhusu mada ya „Uhuru maana yake ni kua huru“. Wimbo utoe jibu au uoneshe nini maana ya Uhuru. Watu kupenda kuishi huru, kuthamini uhuru na sio kuchukulia poa uhuru. Kutoa matumaini kua, siku moja watu wote wataweza kuishi huru na kujisikia pia huru.

Zawadi

Sio nyimbo zote zitawekwa kwenye tovuti yetu. Wimbo wako ukiwa kwenye 16 bora utajishindia nafasi kwenye jukwaa letu mtandaoni. Kwa bahati mbaya sana hatuwezi kutoa zawadi ya fedha au Kitu safari hii kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wetu. Ila bado una nafasi nzuri ya kuendeleza kipaji chako na wimbo wako kusikilizwa na watu wengi kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Majaji

Majaji ni wafanyakazi wa Mission EineWelt watakaosikiliza wimbo wako na maudhui. Kisha wataamua kama wimbo huo unafaa kutangazwa kwenye mitandao yake mbalimbali ya jamii. Utapewa taarifa.

Nyimbo pendwa zitakazochguliwa

Nyimbo zitakazoshinda zitapakiwa kwenye jukwaa letu mtandaoni na kua sehemu ya Maonesho ya mada ya „Uhuru maana yake ni kua huru“ mnamo mwaka 2022 na kuendelea. Pamoja na wimbo wa washindi kuoneshwa kwenye hilo jukwaa, zitaoneshwa pia kwenye tovuti yetu na mitandao yetu ya jamii kama (Facebook/Instagram/YouTube) na vyombo vyetu vya habari.

Kwa maswali zaidi?
Tuandikie sisi Uhuru-Team:
uhuru@mission-einewelt.de

Mission EineWelt
Weil es uns bewegt!

Vigezo na masharti ya kushiriki „Uhuru maana yake ni kua huru“:

1. Kushiriki ni kwa watu wote ambao wametimiza miaka 15 na wanavutiwa lazima wa-eleze uhuru wao wa kibinafsi kwa wimbo. Kwa washiriki wa umri chini ya miaka 18 tamko la
idhini kutoka kwa wazazi lazima pia liwasilishwe. Hicho Kielelezo kinaweza kupakuliwa kutoka https://uhuru-freiheit.com.

2. Kila mshiriki/bendi/kikundi wawasilishe wimbo mmoja tuu. Wimbo uwe kwa njia ya Video kama ni kwa Simu ya mkononi ichukuliwe simu ikiwa imelaszwa. Kisha iwasilishwe kwa faili ya video aina ya mp4.

3. Kuwasilisha hiyo video ni kwa kupakia (upload) kwenye jukwaa letu hili https://uhuru-freiheit.com.

4. Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha ni 31.12.2021.

5. Kushiriki ni bure.

6. Majaji watakao sikiliza na kuchagua nyimbo ni wafanyakazi wa Mission EineWelt.

7. Madai ya hakimiliki nje ya shindano hili na nje ya jukwaa letu, hubaki na washiriki.

8. Kuna mpango wa uchapishaji wa Nyimbo na watunga nyimbo zitakazochaguliwa. Washiriki wanakubaliana na hili kwa kushiriki. Washiriki iwe Bendi au wasanii binafsi wanaweza kutajwa kwa majina au Picha zao kuwekwa kwenye Tovuti au mitandao ya jamii ya Mission EineWelt.

9. Nyimbo zitakazo chaguliwa zitachapishwa.

10. Endapo masharti ya ushiriki yatakiukwa, Mission EineWelt ina haki Kuwatenga washiriki katika hili shindano.Watakao tengwa kwenye shindano pia ni washiriki ambao hawajatimiza vigezo au wanaotumia njia zisizo za haki au kujitambulisha kwa uongo kusudi wafaidike na shindano hili.

11. Mission EineWelt ina haki muda wowote wa shindano hili kuairisha, kukatisha au kusitisha shindano bila kutoa taarifa ya awali wala sababu. Mission EineWelt itatumia hii haki, endapo kutakua na tatizo la kiufundi kwenye mfumo wao wa mtandao kwa mfano kompyuta kuingilwa na virusi, uhalifu au kutokana na sababu za kisheria zinazokwamisha utekelezaji mzuri wa shindano. Endapo visa hivyo vimetokana na mshiriki au kikundi cha washiriki na kusababisha Shindano lisitishwe, basi Mission EineWelt itamdai fidia ya uharibifu.

12. Mission EineWelt hujitahidi kila wakati kuchapisha na kutoa taarifa sahihi. Mission EineWelt haitahusika kwa taarifa isiyosahihi au kwa makosa ya kiufundi yanayohusiana na mashindano. Washirika hushiriki kwa hiari yao wenyewe na kuwajibika vivyo hivyo.

13. Data zinazohitajika kwa washiriki, zinaendana sambamba na Sera ya faragha ya Mission EineWelt, ambayo inaweza kusomwa inapatikana hapa https://mission-einewelt.de/datenschutz/ Washiriki wa Tamasha au wadhamini wa washiriki wanaweza muda wote kuwasiliana na Mission EineWelt, endapo watapenda kuona, kuhakiki au kufuta taarifa zao zilizohifadhiwa. Hii wanaweza kufanya kwa njia ya posta Postfach 68, 91561 Neuendettelsau au kwa njia ya barua pepe uhuru@mission-einewelt.

14. Sheria itakayotumika ni ya jamhuri ya Ujerumani tuu. Endapo mojawapo ya vifungu hivi ni batili au vitakua batili, haitaathiri moja kwa moja vifungu vingine. Uamuzi wa jaji ndio wa mwisho.

15. Kwa kuwasilisha nyaraka zako za ushiriki, unakubaliana na hivi vigezo na masharti.

16. Uamuzi wa majaji ndio wa mwisho.

Mission EineWelt
Weil es uns bewegt